What do I need to know if my child is expelled?

Parent/carer information

# Ninahitaji kujua nini ikiwa mtoto wangu amefukuzwa masomo?

## Habari kwa mzazi/mlezi

### Kufukuzwa ni nini?

Kufukuzwa ni pale ambapo mkuu wa shule na Mkurugenzi, Uongozi wa Elimu wanamwambia mwanafunzi lazima atoke shuleni na asirudi. Kufukuzwa ni suala kubwa. Jitihada zote zinapaswa kufanywa kusaidia mtoto wako kabla ya uamuzi wa kufukuza kufanywa.

Wakuu wa shule wanaweza kufukuza wanafunzi kwa sababu mbili:

- Wanafunzi wanaonyesha tabia mbaya za wasiwasi na mipango ya kusimamia tabia zao haijapata ufanisi.
- Wanafunzi wanao umri wa miaka 17 au zaidi na hawajashiriki katika kujifunza.

Wakuu watafikiria kuhusu jinsi ya shule imesaidia ujifunzaji wa mtoto wako kwa kuzingatia mahitaji na historia yake kabla ya kuamua kufukuza.

Kabla ya kufukuzwa kutokea, mkuu wa shule atawasiliana nawe kukujulisha anafikiria kufukuza mtoto wako. Atatoa notisi iliyoandikwa ya uwezekano wa kufukuzwa na kukualika wewe na mtoto wako kwenye mkutano ili kutoa sababu na kuzungumza kuhusu kitakachotokea ikiwa atamfukuza mtoto wako. Unaweza kumleta mtu wa usaidizi pamoja nawe kwenye mkutano. Msaidizi huyo anaweza kukupa wewe na/au mtoto wako usaidizi wa kihisia au wa vitendo.

Baada ya tarehe ya notisi iliyoandikwa utakuwa na siku saba za shule kutoa jibu kwa shule na sababu kwani mtoto wako asifukuzwe. Mkuu wa shule atatumia jibu hili kama sehemu ya mchakato wa kufanya uamuzi.

### Nini itatokea kama mtoto wangu akifukuzwa?

Mwalimu mkuu na Mkurugenzi, Uongozi wa Elimu wataamua pamoja kama mwanafunzi atafukuzwa. Katika masaa 24 ya kuamua kufukuza mwanafunzi, mkuu lazima awaambie mwanafunzi na wazazi au walezi wake na kujulisha Idara ya Elimu ya NSW.

Ikiwa mtoto wako ana umri chini ya miaka 17 na anafukuzwa kwa sababu ya tabia yake, mkuu lazima apate shule mpya au mazingira mbadala ili aendelee kusoma katika siku 15 za shule.

Ikiwa mtoto wako ana umri ya miaka 17 au zaidi, wewe na mtoto wako mnapaswa kutafuta chaguzi za kuendelea kujifunza au kubadili kwa kazi.

### Je, Ninaweza kupata taarifa gani kutoka shuleni?

Unaweza kuuliza shule kukupa habari zaidi kuhusu kile kilichotokea na kwa nini. Shule inapaswa kukueleza sababu za kufanya maamuzi yoyote, ni hatua gani zitatokea na nini cha kufanya kama una suala.

### Je, ninaweza kukata rufaa ya kufukuzwa?

Ndiyo, ikiwa unaamini kwamba mkuu na Mkurugenzi, Uongozi wa Elimu ulifanya uamuzi usio wa haki au hakufuata taratibu sahihi. Rejelea Nyenzo ya Rufaa.

Habari kuhusu kutetea kwa ajili ya mtoto wako inapatikana, pamoja na Mkataba wetu wa Jamii ya Shule ambao unaeleza njia za kuwasiliana na shule.

### Je, nifanyaje kutoa malalamiko?

Ikiwa una wasiwasi kuhusu kufukuzwa, maamuzi yaliofanywa au usaidizi uliotolewa tafadhali rejelea tovuti kwa habari zaidi juu ya kutoa lalamiko.

### Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa unataka kuwasiliana na shule na unahitaji usaidizi na Kiingereza tafadhali piga simu kwa huduma ya mkalimani wa simu kwenye 131 450, umwambie lugha gani unayohitaji na mwombe mpigaji simu kupiga simu shuleni. Mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu kukusaidia na mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hii.